JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI

# MIKAKATI YA KUONGEZA USHIRIKI WA WAZAWA KWENYE UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UJENZI

# DONDOO


1 Utangulizi

2 Sababu za Ushiriki Mdogo wa Wazawa

3 Mikakati Kuongeza Ushiriki wa Wazawa

4 Road Map




# UTANGULIZI





**Sekta ya Ujenzi ni nini**

**Umuhimu wa Sekta ya Ujenzi**

**Wadau wa Sekta ya Ujenzi**

**Umuhimu wa Wazawa**

# UTANGULIZI…2

## MIRADI ILIYOSAJILIWA NA CRB (JAN 2013- JUNI 2023)






| Mwaka | Idadi | Thamani (Bilioni) |
|---|---|---|
| 2013 | 3,895 | 3,800 |
| 2014 | 2,497 | 7,980 |
| 2015/16 | 5,025 | 6,735 |
| 2016/17 | 3,619 | 6,655 |
| 2017/18 | 3,333 | 9,437 |
| 2018/19 | 3,470 | 5,319 |
| 2019/20 | 2,997 | 3,294 |
| 2020/21 | 3,432 | 4,698 |
| 2021/22 | 3,863 | 5,572 |
| 2022/23 | 4,708 | 8,148 |
| Jumla | **36,839** | **61,638** |

# UTANGULIZI…3

## Ushiriki wa Wazawa –Miradi iliyosajiliwa na CRB

| Mwaka | Miradi iliyosajiliwa | | Miradi iliyotekelezwa na wazawa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Thamani (Shs. Bilioni) | Idadi | | Thamani | |
| | | | Namba | Asilimia | (Shs. Bilioni) | asilimia |
| **2013** | 3,895 | 3,800 | 3,699 | 95 | 1,800 | 48 |
| **2014** | 2,497 | 7,980 | 2,349 | 94 | 1,658 | 21 |
| **2015/16** | 5,025 | 6,735 | 4,756 | 95 | 2,895 | 43 |
| **2016/17** | 3,619 | 6,655 | 3,480 | 96 | 2,141 | 32 |
| **2017/18** | 3,333 | 9,437 | 3,195 | 96 | 1,884 | 20 |
| **2018/19** | 3,470 | 5,319 | 3,335 | 96 | 2,939 | 45 |
| **2019/20** | 2,997 | 3,294 | 2,881 | 96 | 1,704 | 52 |
| **2020/21** | 3,432 | 4,698 | 3,340 | 97 | 2,075 | 44 |
| **2021/22** | 3,863 | 5,572 | 3,738 | 97 | 3,083 | 58 |
| **2022/23** | 4,708 | 8,148 | 4,578 | 97 | 3,570 | 44 |
| **Jumla/Wastani** | **36,839** | **61,638** | **35,351** | **96** | **23,749** | **40.7** |

# UTANGULIZI…4

## Ushiriki wa Wazawa –Miradi ya TANROADS

### MAKANDARASI


| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Miradi (Na.) | | Thamani (Shilingi) | | Mchango wa Wazawa (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wazawa | Kigeni | Wazawa | Kigeni | |
| 2018/19 | 12 | 7 | 187,778,971,607.21 | 591,543,235,536.70 | 24.10 |
| 2019/20 | 1 | 5 | 18,773,648,627.27 | 813,826,675,334.60 | 2.25 |
| 2020/21 | 1 | 5 | 30,875,311,115.70 | 284,315,051,959.47 | 9.80 |
| 2021/22 | 1 | 19 | 34,662,319,857.00 | 1,461,138,913,886.80 | 2.32 |
| 2022/23 | 2 | 30 | 42,024,002,847.04 | 5,537,893,255,021.50 | 0.75 |
| **Wastani** | **3** | **13** | **62,822,850,810.84** | **1,737,743,426,347.81** | **7.84** |

### WASHAURI ELEKEZI

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Miradi (Na.) | | Thamani (Shilingi) | | Mchango wa Wazawa (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wazawa | Kigeni | Wazawa | Kigeni | |
| 2018/19 | 9 | 7 | 9,733,477,855.40 | 26,803,463,513.63 | 26.64 |
| 2019/20 | 3 | 2 | 1,222,856,343.00 | 1,551,877,484.00 | 44.07 |
| 2020/21 | 5 | 4 | 7,065,000,000.00 | 13,157,741,136.93 | 34.94 |
| 2021/22 | 7 | 10 | 10,247,474,416.85 | 31,112,306,404.83 | 24.78 |
| 2022/23 | 4 | 6 | 6,784,616,325.10 | 18,023,975,517.50 | 27.35 |
| **Wastani** | **6** | **6** | **7,010,684,988.07** | **18,129,872,811.38** | **31.60** |

# UTANGULIZI…5

## MJENGEKO WA BEI YA MKANDARASI



Faida (5%)

Risk (2%)

Uweke zaji (0.5%)

Site Overhead (12.5%)

Office Overhead (2%)

Materials (38%)

Mitambo (28%)

Wafany akazi (12%)

# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA ---1



## Masharti Magumu Kwenye Zabuni


1. Wastani wa Mapato Ghafi ya Mwaka (Average Annual Turnover)
2. Dhamana ya Zabuni (Tender Security)
3. Dhamana ya Utekelezaji Kazi (Performance Security)
4. Uzoefu wa Kazi zinazofanana (Specific Experience in Similar Works)
5. Mtaji wa Kutekeleza Kazi (Working Capital)
6. Mitambo (Plants and Equipment)

# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA ---2

**Kuchelewa malipo kwa makandarasi na washauri elekezi**

1. Malipo kuchelewa

2. Kuondolewa riba ya ucheleweshaji (interest on delayed payment) kwenye mikataba



# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA ---3



**Masharti magumu na riba kubwa ya upatikanaji wa mitaji**

1. Riba ni kubwa wastani wa 18% inayosababisha gharama kubwa ya mtaji na kushindwa kushindana na wageni

2. Mabenki yanahitaji kuweka dhamana ya mali isiyoondosheka

3. Mikopo ya muda mfupi isiyohitahi dhamana (unsecured loan) huwa kiwango kidogo, mfano CRBD Bank ukomo ni TZS 2 Billioni kwa mkataba mmoja.

# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA --- 4

**Kutotengwa kwa miradi mingi kwa ajili ya kukuza uwezo wa makandarasi wazawa**

1. Miradi hii huwezesha Makandarasi kujenga kukuza ujuzi na uzoefu wa kazi kubwa na hivyo kufikia vigezo vya kutekeleza miradi mikubwa

2. Miradi hii huwa na programu ambapo timu ya watalaam hufuatilia utekelezaji wa makandarasi kwa lengo la kutatua changamoto zozote wanazokumbana nazo na hivyo kujenga uzoefu na ujuzi wa kutekeleza miradi mikubwa

3. Hukuza mitaji, uzoefu, utaalamu, mitambo na menejimenti ya miradi mikubwa

4. Hukuza mahusiano mazuri na washitiri na wandarasi wenzao



# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA ... 5



**Makandarasi na washauri elekezi kutoa bei za chini isivyo kawaida (abnormally low) katika zabuni**

1. Hii inatokana na ushindani mkubwa uliopo, hivyo ili kupata kazi, hutengeneza zabuni zenye bei ndogo
2. Mara nyingi hushindwa kutekeleza miradi na kuharibu zifa za kampuni yake na za wazawa
3. Au hutekeleza kwa kusukumana sana na wasimamizi na hivyo kuharibu mahusiano na washitiri na wasimamizi wa miradi
4. Au kutekeleza chini ya kiwango, kupata hasara na hivyo kusababisha woga kwa wengine.

# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA... 6

**Wadau wa maendeleo kutotambua upendeleo wa makandarasi wa ndani katika miradi wanayoifadhili**

1. Upendeleo katika tathmini ya zabuni ambazo mzawa angepewa ahueni ya hadi 10% (margin of preference) haupo

2. Takwa la kulazimisha mashirikiano kati ya wageni na wazawa halipo

3. Miradi kugawanywa ili kuwezesha wazawa kufaulu zabuni

4. Hitaji la shortlist ya washauri elekezi kutoka katika bara



# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA ... 7



**Kutokuwepo na Mpango Maalumu wa Kuwaendeleza Wataalamu na Makandarasi wa Ndani**

1. Mpango mahsusi wenye dhumuni la kuendeleza wazawa
2. Wenye malengo ya idadi, ubora, na muda wa kuyafikia malengo hayo
3. Wenye rasilimali za kuutekeleza
4. Uliogawanya majukumu kwa wadau mbalimbali
5. Wenye kufanyiwa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini

# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA ... 8

**Sera ya Ujenzi ya Taifa ya Mwaka 2003 kutakiwa kufanyiwa mapitio**

1. Kuwa na tathmini ya ushiriki wa wazawa katika kutekeleza miradi ya ujenzi nchini

2. Kuwa na madhumuni na malengo mahsusi ya kuongeza ushiriki wa wazawa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi nchini

3. Kuwa matamko mahsusi ya kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye miradi (local content statements)



# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA ... 9



**Ubinafsi miongoni mwa Makandarasi na Washauri Elekezi Wazawa**

1. Sababu kubwa ya kutoshindana na wageni ni uwezo wetu mdogo
2. Tungeungana tungeboresha uwezo wetu na kuweza kushindana na pia tungeweza kujengeana uwezo
3. Umoja ni nguvu utengano ni dhaifu
4. Tunapoungana tunaungana changamoto ni nyingi

# SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WAZAWA --- 10

**Mtazamo wa Taasisi Nunuzi (PE's) kuhusu makandarasi na washauri elekezi wazawa**

1. Hawatekelezi kazi bila kusukumana
2. Hawatekelezi kazi kwa viwango vinavyohitajika
3. Menejimenti ya rasilimali za mradi ni hafifu
4. Huleta kufahamiana kwenye masuala ya kazi
5. Hivyo vipengele vya upendeleo (Prefential Schemes) havitumiki



## MIKAKATI KWA UJUMLA



Kuboresha masharti na vigezo katika zabuni za ujenzi na washauri elekezi



Kuhakikisha malipo ya miradi yanalipwa kwa wakati au kufidiwa riba ya ucheleweshaji



Kutenga miradi ya kujenga uwezo wa wakandarasi kila mwaka na kufuatilia utekelezaji wake



Kuhakikisha miradi yote mikubwa inatekelezwa kwa kushirikisha wazawa

# MIKAKATI KWA UJUMLA



Kufanya mapitio ya Sera ya Ujenzi na Kuandaa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta



Kushawishi Mabenki kutoa mikopo kwa masharti rafiki



Kuandaa Miongozo ya gharama msingi za ujenzi kwa kila kazi ya ujenzi (base unit rates) kwa kila mkoa



Kushawishi Wadau wa Maendeleo kuruhusu kujenga uwezo kwa wazawa

# MIKAKATI KWA UJUMLA



Kuongeza mtaji katika Mfuko wa Kusaidia Wakandarasi (CAF)



Kuwa na programu maalum na ya makusudi ya kujenga uwezo wa wakandarasi, washauri elekezi na wataalam wazawa ili kuweza kushindana kimataifa



Kuendelea kujenga uwezo wa taasisi nunuzi katika masuala ya ununuzi na usimamizi wa miradi ya ujenzi



Kuweka Mfumo wa "Local Content" (Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo rasm) kwa sekta ya ujenzi

# Kuboresha Vigezo na Masharti katika Zabuni za Miradi ya Ujenzi





- **Wastani wa Mapato Ghafi kwa Mwaka (Average Annual Turnover**

1. Kigezo cha mapato ghafi ya mwaka kiendelee kuanishwa kama kigezo muhimu cha kupima uwezo wa mzabuni kutekeleza mradi husika.

2. Kwa miradi itakayotengwa kwa ajili ya kujenga uwezo Kiwango cha wastani wa mapato ya mwaka (average annual turnover) kisizidi 50% ya makisio ya thamani ya kazi kwa mwaka (estimated annual project implementation cost of contract).

# Kuboresha Vigezo na Masharti katika Zabuni za Miradi ya Ujenzi





- **Kiwango cha Dhamana ya Zabuni (Tender Security)**

1. Tamko la Dhamana (Tender Securing Declaration) itumike kwa miradi ya thamani hadi ukomo wa upendeleo wa kampuni za ndani (Local Exclusive Preference), na miradi itakayotengwa kwa ajili ya kujenga uwezo wa wazawa

- **Kiwango cha Dhamana ya Utekelezaji wa Kazi (Performance Security)**

- Taasisi Nunuzi zitatumia aina zote tatu za dhamana yaani kutumia dhamana za benki (Performance guarantee), dhamana za bima (Performance bond) au Tamko (Performance Securiting Declaration) kulingana na viashiria vya hatari vya mradi na mkandarasi husika (risk based).

# Kuboresha Vigezo na Masharti katika Zabuni za Miradi ya Ujenzi





## Uzoefu wa Kazi zinazofanana (Specific Experience in Similar Works)

i) Kuandaa kwa kina na kuwasilisha kazi alizofanya zenye kufanana na kazi zitakazotekelezwa kwenye mradi husika kwa kuzingatia mbinu za ujenzi na teknolojia inayotumika zinawiana;

ii) Kuandaa na kuwasilisha andiko la jinsi atakavyotekeleza mradi husika (construction methodology) akielezea kwa kina jinsi atakavyotekeleza mradi huo hatua kwa hatua kuanzia mwanzo hadi mwisho; na

iii) Kuandaa na kuwasilisha taarifa za watalaamu watakaotumika katika kutekeleza mradi husika, wasifu (CVs.)

iv) CRB, ERB, AQRB na NCC zitawajengea uwezo makandarasi na washauri elekezi wazawa katika maandalizi ya zabuni shindani.

# Kuboresha Vigezo na Masharti katika Zabuni za Miradi ya Ujenzi





## Mitambo

i) Nyaraka za Zabuni zinazoandaliwa na taasisi nunuzi ziainishe mahitaji ya mitambo inayoendana na mahitaji halisi ya kazi husika;

ii) Katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali kwa kupitia NCC, CRB na TEMESA kufanya tafiti ya mahitaji halisi ya mitambo na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kukidhi mahitaji hayo; na

iii) CRB, TEMESA na NCC kuwajengea uwezo makandarasi wazawa katika menejimenti ya mitambo ya ujenzi.


# Kuboresha Vigezo na Masharti katika Zabuni za Miradi ya Ujenzi





- Kwa miradi ya kati na mikubwa (Medium and Large Works)
  - Miradi hadi Shilingi Bilioni 50 itatengwa kwa ajili ya Makandarasi wa ndani
  - Miradi yote itakayotekelezwa na Makandarasi wa Kigeni lazima washirikiane (sub-contract) na Makandarasi Wazawa
  - Taasisi Nunuzi kuainisha utaratibu na sifa za makandarasi wanaostahili kupewa sub-contract
  - Kwa kuanzia TANROADS ianishe kazi zote zinaweza kutengwa kwa ajili ya sub-contracting ili ziwekwe kwenye mfumo wa NeST.
  - Kuwe na ukomo wa idadi ya miradi mkandarasi mmoja anayoweza kupewa kama sub-contractor kwa ajili ya kujenga uwezo

## Kuboresha Vigezo vya Zabuni za Miradi ya Ujenzi





- Kwa upande wa zabuni za miradi ya midogo (Small Works)
  - **Taasisi Nunuzi zinaweza kutumia dhamana yoyote kati ya Tamko la dhamana (performance Securing Declaration), dhamana ya benki, au dhamana ya bima**
  - **TANROADS inaweza kuainisha kazi ambazo kampuni mpya za Kikandarasi zinaweza kupewa ili ziingizwe kwenye mfumo wa NeST**

## Kuboresha Vigezo vya Zabuni za Miradi ya Ushauri Elekezi

## Zabuni za Washauri Elekezi



- Ili kuongeza ushiriki wa makampuni na watalaam washauri elekezi wa ndani pia TANROAD imefanyia maboresho kwenye vigezo ya kuitisha zabuni za kupata washauri elekezi (request for proposal).

- Zabuni za ushauri elekezi, zimefanyiwa mapendekezo ya maboresho kama inavyooneshwa katika Slide inayofuata

| UPEMBUZI YAKIBNIFU NA USANIFU WA KINA | | | |
|---|---|---|---|
| | **Wataalamu** | **Vigezo vya Ushiriki** | **Mabadiliko** |
| 1 | Kiongozi wa Timu (Team Leader) | • uzoefu wa jumla ya miaka kumi (10) unaohusu usanifu wa barabara.<br>• Uzoefu katika nafasi husika angalau kwa miradi 2 inayofanana na mradi husika katika miaka 10 iliyopita. | • uzoefu wa jumla ya miaka kumi (10) unaohusu usanifu wa barabara.<br>• Uzoefu katika nafasi husika angalau kwa miradi 2 inayofanana na mradi husika katika miaka 10 iliyopita akiwa amefanya kazi kwa Mshitiri (Client), Mkandarasi (Contractor) au Mshauri Elekezi |
| 2 | Wataalamu Wengine (Other Key Staff) | • Uzoefu wa miaka 6 wa kazi zinazohusiana na usanifu wa barabara.<br>• Uzoefu katika nafasi husika angalau kwa miradi 2 inayofanana na mradi husika katika miaka 10 iliyopita. | • Uzoefu wa miaka 6 wa kazi zinazohusiana na usanifu wa barabara.<br>• Uzoefu katika nafasi husika angalau kwa miradi 2 inayofanana na mradi husika katika miaka 10 iliyopita akiwa amefanya kazi kwa Mshitiri (Client), Mkandarasi (Contractor) au Mshauri Elekezi |
| 3 | Wataalamu wa Mazingira na Jamii (Environmental and Social Experts) | • Uzoefu wa jumla wa miaka 5 katika madhara kwa jamii na mazingira, masuala ya ukatili wa kijinsia na uzoefu wa kiuendeshaji.<br>• Uzoefu katika nafasi nafasi husika katika miradi 2 ya 'ESIA na Social Study' na masuala yanayohusu Ukatili wa Kijinsia (GBV) kwenye mradi 1 unaofanana na mradi husikandani ya miaka 5 iliyopita. | • Uzoefu wa jumla wa miaka 5 katika madhara kwa jamii na mazingira, masuala ya ukatili wa kijinsia na uzoefu wa kiuendeshaji.<br>• Uzoefu katika nafasi nafasi husika katika miradi 2 ya 'ESIA na Social Study' na masuala yanayohusu Ukatili wa Kijinsia (GBV) kwenye mradi 1 unaofanana na mradi husikandani ya miaka 5 iliyopita akiwa amefanya kazi kwa Mshitiri (Client), Mkandarasi (Contractor) au Mshauri Elekezi |

| Na. | Wataalamu | Vigezo vya Ushiriki | Mabadiliko |
|---|---|---|---|
| | | **USIMAMIZI WA MIRADI** | |
| **1.** | Mhandisi Mkazi (Resident Engineer) | • Uzoefu wa jumla ya miaka 12 unaohusu ujenzi wa barabara.<br><br>• Uzoefu katika nafasi husika katika miradi 2 inayofanana na mradi husika ndani ya miaka 10 iliyopita. | • Uzoefu wa jumla ya miaka 12 unaohusu ujenzi wa barabara.<br><br>• Uzoefu katika nafasi husika katika miradi 2 inayofanana na mradi husika ndani ya miaka 10 iliyopita akiwa amefanya kazi kwa Mshitiri (Client), Mkandarasi (Contractor) au Mshauri Elekezi |
| **2.** | Wataalamu Wengine Muhimu (Other Key Staff) | • Uzoefu wa miaka 8 katika miradi ya ujenzi wa Barabara<br><br>• Uzoefu katika nafasi husika katika miradi 2 inayofanana na mradi unaoshindaniwa ndani ya miaka 10 iliyopita. | • Uzoefu wa miaka 8 katika miradi ya ujenzi wa Barabara<br><br>• Uzoefu katika nafasi husika katika miradi 2 inayofanana na mradi unaoshindaniwa ndani ya miaka 10 iliyopita akiwa amefanya kazi kwa Mshitiri (Client), Mkandarasi (Contractor) au Mshauri Elekezi. |
| **3.** | Wataalamu wa Mazingira na Jamii (Environmental and Social Experts) | • Uzoefu wa jumla wa miaka 5 katika madhara kwa jamii na mazingira, masuala ya ukatili wa kijinsia na uzoefu wa kiuendeshaji katika miradi.<br><br>• Uzoefu katika nafasi husika katika miradi 2 ya 'ESIA na Social Study' na masuala yanayohusu Ukatili wa Kijinsia (GBV) kwenye mradi mmoja (1) unaofanana na mradi unaoshindaniwa ndani ya miaka 5 iliyopita. | • Uzoefu wa jumla wa miaka 5 katika madhara kwa jamii na mazingira, masuala ya ukatili wa kijinsia na uzoefu wa kiuendeshaji katika miradi.<br><br>• Uzoefu katika nafasi husika katika miradi 2 ya 'ESIA na Social Study' na masuala yanayohusu Ukatili wa Kijinsia (GBV) kwenye mradi mmoja (1) unaofanana na mradi unaoshindaniwa ndani ya miaka 5 iliyopita akiwa amefanya kazi kwa Mshitiri (Client), Mkandarasi (Contractor) au Mshauri Elekezi |

## Kutenga Miradi Maalum kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Wazawa

### Mkakati



Mpango maalum wa miaka mitano (5) wa kukuza uwezo na ushiriki wa wazawa katika kazi za ujenzi wa barabara na madaraja kama ifuatavyo: -

a) Kutenga asilimia kumi (10%) ya bajeti ya kila mwaka ya maendeleo kwa ajili ya Miradi ya mafunzo kwa vitendo kwa Makandarasi Wazawa ili kuwajengea uwezo. Katika mafunzo hayo inapendekezwa kuwa Makandarasi wazawa wapewe elimu ya darasani kama vile maandalizi ya zabuni ikiwemo kuandaa bei halisi za kazi husika, tafsiri ya vifungu vya nyaraka za zabuni na mikataba, usimamizi wa raslimali kama vile fedha, mitambo/vifaa na raslimali watu katika utekelezaji wa miradi;



a) Kutenga angalau asilimia thelathini (30%) ya bajeti ya maendeleo kwa ajili ya upendeleo kwa wazawa (local exclusivity) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi iandae mwongozo wa namna ya kutekeleza miradi ya kujenga uwezo kwa wazawa. Mwongozo huu ni muhimu kwa ajili ya kuweka utaratibu mzima wa kutenga miradi, namna ya kuitekeleza, masuala ya ufuatiliaji na tathmini;

# Kutenga Miradi Maalum kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Wazawa...2





## Mkakati...2


- Kutenga angalau asilimia tano (5%) ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya makundi maalum Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi

- Wizara itaandaa mwongozo wa namna ya kutekeleza miradi ya kujenga uwezo kwa kundi maalum. Mwongozo huu ni muhimu kwa ajili ya kuweka utaratibu mzima wa kutenga miradi, namna ya kuitekeleza, masuala ya ufuatiliaji na tathmini;

- Miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na ile ya Usimamizi (Supervision) inayotumia fedha za ndani ya nchi itekelezwe na makampuni ya Washauri elekezi wa ndani

# Kutenga Miradi Maalum kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Wazawa...3





## Mkakati ... 3

a) Miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na Usimamizi (Supervision) inayotumia fedha za mikopo na misaada itatekelezwa kutekelezwa kwa ushirikiano kati Washauri Elekezi wazwa na wale wa nje;

a) Ushiriki wa wanafunzi na wahitimu katika miradi. Inapendekezwa Wakala kutoa nafasi za ushiriki wa mafunzo kwa wanafunzi na wahitimu 1,500 wa fani za uhandisi kama vile SEAP na fani zingine katika miradi inayotekelezwa na TANROADS.

a) Kazi za matengenezo ya barabara na madaraja zitekelezwe na Makandarasi Wazawa na kusimamiwa na Washauri Elekezi Wazawa tu.

# Kutenga Miradi Maalum kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Wazawa...4







## Mikakati…4

- Kazi za matengenezo ya barabara na madaraja zitekelezwe na Makandarasi Wazawa na kusimamiwa na Washauri Elekezi Wazawa tu.

- Mpango unaopendekezwa kutekelezwa ili kuongeza ushiriki wa Wazawa katika miradi katika kipindi cha miaka mitano ijayo umeoneshwa kwenye **slide inayofuata**

| No | Mikakati | | Lengo la mwaka 2024/25 – 2029/30) |
|---|---|---|---|
| 1. | Kutenga fedha za Miradi ya mafunzo kwa vitendo kwa Makandarasi Wazawa ili kuwajengea uwezo | | Kutenga 10% ya bajeti maendeleo kwa ajili ya Miradi ya kujenga uwezo wa Makandarasi Wazawa |
| 2. | Kutenga fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya upendeleo kwa Makandarasi wazawa (local exclusivity) | | 30% ya bajeti ya maendeleo kwa ajili ya upendeleo kwa wazawa (Local Exclusive Projects) |
| 3. | Kutenga fedha za bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya Makandarasi Wanawake | | 5% ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa wanawake |
| 4. | Miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na ile ya Usimamizi (Supervision) inayotumia fedha za ndani ya nchi | | Itekelezwe na makampuni ya Washauri elekezi wa ndani |
| 5. | Miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na Usimamizi (Supervision) inayotumia fedha za mikopo na misaada | | kutekelezwa kwa ushirikiano kati Washauri Elekezi wa ndani na wale nje |
| 6. | Ushiriki wa wanafunzi na wahitimu katika miradi | | Angalau wanafunzi na wahitimu 300 kila mwaka katika miradi inayotekelezwa na TANROADS. |
| 7. | Kazi za matengenezo ya barabara na madaraja | | Zitekelezwe na Makandarasi Wazawa na kusimamiwa na Washauri Elekezi wandani tu. |

# Miradi inayofadhiliwa na Wadau wa Maendeleo





## Mikakati

1. Serikali imeanza mazungumzo ya wadau wa maendeleo (WB na AfDB) ili kutambua nia ya kujenga uwezo wa wazawa

2. Suala la local content kwenye kila Maandiko ya miradi inayopendekezwa kufadhiliwa na Wadau wa Maendeleo. Hivyo, katika Maandiko ya miradi (project appraisal document) vifungu vya upendeleo wa makandarasi na washauri elekezi wa ndani vitapewa kipaumbele.

3. Maandiko ya miradi kuwe na kifungu maalum (sub-component) cha kujenga uwezo (capacity building) wa makandarasi na washauri elekezi wa ndani katika miradi ya wafadhili.

# Masharti Magumu ya Kupatikana Mitaji





1. Serikali inakusudia kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (CAF) kwa kuwekeza mtaji (ifikie angalau Shilingi Bilioni100 ndani ya miaka mitano (5)) ili uwe na uwezo wa kuwadhamini makandarasi wengi wazawa.
    - Serikali kutunga sheria itakayowezesha kutenga kiasi cha Shilingi Bilioni 20 kila mwaka kwa ajili ya kutunisha mfuko huu .
    - Benki zitakazokuwa zinasimamia mfuko huu zitatakiwa kuweka kiwango sawa na kiwango cha Serikali katika akaunti ya Mfuko katika benki hiyo kwa wakati huo.

2. Serikali inaendelea na majadiliano na benki ili kutambua mikataba ya kazi kama dhamana kwa kuingia makubaliano (MoU) baina ya Benki, Taasisi Nunuzi na Mkandarasi kupitisha malipo yote ya kazi husika kwenye akaunti ya mkandarasi katika benki husika. Mpango huu utawezesha makandarasi kupata mikopo ya muda mfupi kwa dhamana za mikataba ya ujenzi waliyoingia.


## Kukamilisha Miongozo ya Gharama za Ujenzi wa Barabara





- Ili kuondoa changamoto ya makandarasi wazawa kutoa bei za chini kupindukia, NCC kwa kushirikiana na RFB inaandaa Mwongozo wa Gharama za Ujenzi na Ukarabati wa Barabara ambao utatumiwa na TANROADS kuandaa makisio ya gharama za miradi.
- Imeandaliwa kwa kutumia kanuni za msingi (first principles) za uandaaji gharama
- Kazi zote kwa kila mkoa zitakuwa na gharama yake
- Mwongozo huu unatarajiwa kuwa umekamilika hadi kufikia mwezi wa 12 mwaka 2024.
- Makandarasi watafundishwa namna ya kutumia mwongozo huu pia kuandaa bei zao za miradi na hivyo kupunguza changamoto ya kuwasilisha zabuni zenye bei ndogo kupindukia.

## Kufanya Mapitio ya Sera ya Ujenzi na Kuandaa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ujenzi Nchini



Wizara ya Ujenzi itakamilisha mapitio ya Sera ya Ujenzi ya Mwaka 2003 kabla au ifikapo mwezi Juni 2025. Inatarajiwa mapitio ya Sera ya Ujenzi yatatoa fursa ya kuongeza matamko ya Local Content katika Sera hiyo. Aidha katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Ujenzi itaandaa Mpango Mkakati wa Miaka 10 wa Kuendeleza Sekta ya Ujenzi nchini. Katika Mpango Mkakati huu malengo mbalimbali ya kuendeleza wazawa yataainishwa sambamba na mgawanyo wa majukumu kwa wadau wa sekta ili kufikia malengo hayo.

## Kujenga Uwezo wa Washauri Elekezi kupitia Kuanzisha Shule ya Uhandisi




- Serikali kwa kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) inatarajia kuanzisha Shule ya Uhandishi (School of Engineering) ambayo itakuwa na jukumu la msingi la kujenga uwezo wa watalaam wahandisi ili waweze kuwa na sifa zinazohitajika kutekeleza miradi ya ujenzi mikubwa kama washauri elekezi. Shule hii inatarajia kuanza rasmi katika mwaka wa fedha 2024/2025.
-

# Ubinafsi miongoni mwa makandarasi na washauri elekezi wazawa.



- Serikali kupitia AQRB, CRB, ERB na NCC kuendelea kujenga uwezo wa watalaam na makampuni ya wazawa umuhimu wa kuunda ushirikiano.

- Watalaam wa taasisi hizi, kuendelea kutoa ushauri pindi mashirikiano hayo yakianzishwa na kushinda mkataba

# Mtazamo hasi wa Taasisi Nunuzi (PE’s) kwa makandarasi na washauri elekezi wa ndani




- Serikali kwa kupitia PPRA ikishirikiana na AQRB, CRB, ERB na NCC itaendelea kutoa elimu kwa taasisi nunuzi ili ziweze kutekeleza sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 ipasavyo hasa katika vifungu vinavyotoa upendeleo kwa makandarasi na washauri elekezi wa ndani.

## Kuweka Mfumo wa Kisera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Local Content kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi





- Wizara ya Ujenzi kwa kupitia taasisi zake za AQRB, CRB, ERB, NCC, RFB, TANROADS na TBA inaandaa Andiko Dhana la kupendekeza kutungwa Matamko ya Local Content katika Sera zote zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi pamoja na katika Sera ya Ununuzi wa Umma. Aidha, Andiko Dhana hilo pia litapendeza umuhimu wa kutungwa Sheria ya Local Content kwa ajili ya shughuli za Sekta ya Ujenzi.
- Mfumo wa Kisera na Kisheria ndio pekee utakaoweza kuhakikisha utekelezaji endelevu wa mikakati ya kuongeza ushiriki wa wazawa katika miradi ya ujenzi.
-

# DIRA






- lengo kuu ni kuwajengea uwezo hatua kwa hatua wakandarasi, washauri elekezi na watalaam wazawa ili waweze kutekelea miradi mikubwa ya ndani na hatimaye kushindana kimataifa.
- Hadi ifikapo Juni 30, 2025 Sheria, Sera na Mpango Mkakati wa kuendeleza Sekta ya ujenzi ziwe zimekamilika
- Hadi ifikapo Juni 30 2030, asilimia 65 ya thamani ya miradi yote ya ujenzi iwe inatekelezwa na Wazawa
- Hadi ifikapo Juni 30, 2030, asilimia 50 ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na TANROADS itekelezwe na wazawa
- Hadi ifikapo Juni 30, 2035, asilimia 80 ya thamani ya miradi yote ya ujenzi iwe inatekelezwa na Wazawa, asilimia 75 ya miradi maendeleo inayotekelezwa na TANROADS itekelezwe na wazawa


ASANTE SANA